

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA  
MTIHANI WA UALIMU DARAJA A**

**689**

**VITENDO VYA KUJIFUNZA SAYANSI**

**Muda: Saa 3**

**Mwaka: 2020**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenyе jumla ya maswali **kumi na sita (16)**.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na maswali **mawili (2)** kutoka kila sehemu B na C.
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B na C zina alama **thelathini (30)** kila moja.
4. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



### **SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. (a) Bainisha mambo manne yanayoweza kusababisha mtoto kupata ajali.  
(b) Taja tahadhari nne za kuchukua ili kumwepusha mtoto kupata ajali.
2. (a) Orodhesha magonjwa manne ambayo watoto wa Elimu ya Awali wanaweza kuambukizana wakikaa pamoja.  
(b) Bainisha magonjwa manne ambayo mtoto akiugua yanaweza kumsababishia ulemavu.
3. (a) Bainisha sifa nne za maji.  
(b) Taja madhara manne anayoweza kupata mtoto kwa kutumia maji machafu.
4. (a) Kwa nini inashauriwa watoto wa Elimu ya Awali kufundishwa kwa vitendo zaidi? Toa hoja nne.  
(b) Je, mtoto hujifunza kwa kutumia milango ipi ya fahamu?
5. (a) Chakula bora ni chakula cha aina gani?  
(b) Ainisha madhara matatu yanayoweza kujitokeza iwapo mtoto hatapewa chakula bora.
6. (a) Bainisha vyanzo viwili vya joto na matumizi yake katika maisha ya kila siku.  
(b) Taja matendo manne ambayo mtoto wa darasa la Elimu ya Awali anaweza kufanya wakati wa baridi ili kuondoa baridi mwilini mwake.
7. Misingi ya kufundishia na kujifunzia ina umuhimu gani kwa wanafunzi wa elimu ya awali? Toa hoja nne.
8. Ni ilani zipi hutolewa kwa njia ya maandishi katika mazingira tunayoishi? Toa hoja nne.
9. Fafanua kwa ufupi vipengele vinne vya kwanza katika uandishi wa ripoti ya jaribio la kisayansi.
10. Kwa nini baadhi ya watoto huwa wachafu muda wote? Eleza kwa kifupi kwa kutoa hoja nne.

### **SEHEMU B (Alama 30)**

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

11. Mtoto wa elimu ya awali anatakiwa kushirikishwa kikamilifu katika utunzaji wa mazingira ya shule. Ukiwa mwalimu tarajali wa Elimu ya Awali, thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kutumia hoja sita.

12. Wazazi na walezi wana jukumu la kuhakikisha kuwa watoto wanaepukana na maambukuzi ya magonjwa. Eleza mambo sita ambayo watoto wanatakiwa kufanyiwa ili waepukane na maambukizi ya magonjwa.
13. (a) Eleza hatua tano utakazotumia kumwelekeza mtoto wa Elimu ya Awali namna bora ya kupiga pasi nguo zake,
- (b) Fafanua matumizi ya vifaa mbadala vitatu utakavyowafundisha watoto wa Elimu ya Awali kutumia kusafisha kinywa na meno.

### SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

14. (a) Kwa kutumia hoja mbili, eleza umuhimu wa upimaji kwa watoto wa elimu ya awali.
- (b) Fafanua aina tatu za upimaji na umuhimu wake kwa watoto wa Elimu ya Awali.
15. Changanua mbinu sita zinazofaa kuwafundishia watoto wa Elimu ya Awali mada ya Usafi wa Mwili.
16. Kubaini suala la utafiti ni jambo la msingi kabla ya kuanza mchakato wowote wa kufanya utafiti. Bainisha sifa sita za suala bora la utafiti.